# MATUMIZI YA MISIMU KWA WAZUNGUMZAJI WA KISWAHILI KATIKA VYUO VIKUU NCHINI TANZANIA: UCHUNGUZI KIFANI WA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

***Editha Adolph***
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Tanzania*
petereddy51@gmail.com

## Ikisiri

*Makala hii inachunguza matumizi ya misimu kwa wazungumzaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Tanzania, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kikichukuliwa kama mfano unaowakilisha vyuo vingine. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa matini, hojaji na usaili. Mbinu ya kuchambua matini ilijumuisha usomaji wa majarida, nyaraka za kitaaluma mathalani, tasinifu, kamusi na nyaraka zinazohusiana na mada husika. Aidha, mbinu ya hojaji ilijumuisha hojaji, ambapo ziligawiwa kwa wanachuo 20 wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambacho kinapatikana katika Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam. Aidha, mtafiti ametumia usaili kama mbinu nyingine ya kupata data ya makala hii. Nadharia iliyoongoza makala hii ni* Nadharia *Jumuishi ya Giles (1979).* Halikadhalika, *mkabala wa kitaamuli au maelezo ulitumika kuchambulia data ya makala hii. Licha ya suala la misimu kuangaziwa na Malima (2018) ambaye alichunguza misimu inayotumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu vya Mkoa wa Morogoro katika mitandao ya kijamii, bado kuna haja ya kuangazia suala hilo katika vyuo vikuu kwa kutumia mazingiria na muktadha mwingine tofauti, wa kuchunguza matumizi ya misimu katika mawasiliano ya wanafunzi ya kawaida wakiwa katika mazingira ya Chuo Kikuu na sio katika mitandao ili kujua kinagaubaga aina ya misimu inayoibuliwa. Matokeo yameonesha kuwa misimu inayotumiwa na wanachuo hao hupatikana katika nyanja mbalimbali: taaluma, uchumi pamoja na jamii. Maana ya misimu hiyo imeoneshwa kutokana na majibu ya watoa taarifa wa makala hii. Makala hii inapendekeza vyombo vinavyosimamia Kiswahili (k.v.*

*BAKITA na BAKIZA) kuchunguza misimu hiyo na kuona kama kuna baadhi inafaa kusanifishwa.*

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu mbalimbali kama Sengo (1973), Spears (1991), Dalzell (2006), Almas (2011), Ibrahim (2012), TUKI (2013), Shayo (2015) na Kiunga (2016) wanakubaliana kuwa misimu ni maneno yenye uficho, yanayozuka katika jamii na kutumiwa na watu ambao huelewana. Kipacha (2003) anaongeza kuwa misimu inayodumu huweza kuingia katika methali, nahau au misemo ya lugha ya jamii husika. Njoka (2004) kwa upande wake anaona kuwa misimu ni jumla ya maneno yote ambayo siyo sanifu katika lugha yoyote ile, mathalani Kiswahili. Maneno hayo yameibuliwa na vikundi vidogo vya watu wenye utamaduni unaofanana kwa lengo la kuwa na usemi mmoja unaolinda mawazo na mawasiliano miongoni mwao. Sababu ya kuitwa misimu ni kuwa maneno hayo huzuka na kupotea kulingana na matukio fulani katika jamii husika. Wapo wataalamu waliochunguza matumizi ya misimu; mathalani, Msanjila (2009) anaona kuwa misimu hutumiwa kama siri miongoni mwa wanajamii kwa kuwa wanaelewa maana ya maneno au semi husika. Anatoa mfano wa msimu *sonko* wenye maana ya tajiri, *piga ngeta* wenye maana ya kumwibia mtu kwa kumvizia na kumkaba. King'ei (2010) naye kwa upande wake anaona kuwa matumizi ya misimu miongoni mwa wanajamii huweza kusababisha kuvunjwa kwa kanuni za lugha sanifu. Mtazamo huu una ukweli ndani yake kwani imeelezwa hapo awali kuwa misimu ni maneno yasiyosanifishwa, yanayozuka miongoni mwa wanajamii ambapo baadhi yake hushika mizizi na kusanifishwa na mengine hutoweka. Fasili hii inaunga mkono mawazo ya King'ei (keshatajwa) kutokana na ukweli kuwa maneno haya hutumika pasipo kuhakikiwa na wakuza lugha na hivyo, hutumika pasipo kusanifishwa. Hivyo, ni dhahiri kuwa maneno haya husababisha kuvunjwa kwa kanuni za lugha sanifu.

Thorne (2015) anadai kuwa hadi mwishoni mwa karne ya 16 matumizi ya misimu yalishika kasi na kuwa kama lugha ya kawaida. Mtaalamu huyu anasema kuwa, kufikia karne ya 18 wanafunzi walifundishwa kutotumia misimu katika lugha ya Kiingereza. Pamoja na angalizo hilo, miaka ya 1700 kulikuwa na matukio mbalimbali yaliyosababisha kuwapo kwa matumizi ya misimu huko Uingereza na Amerika. Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na hali ngumu ya uchumi, magonjwa, njaa, mafuriko, na kadhalika yaliyosababisha kuzuka na kutumika kwa misimu mbalimbali.

Malima (2018) kwa upande wake, alishughulikia matumizi ya misimu ya lugha kwenye mitandao ya kijamii kwa wazungumzaji wa Kiswahili katika vyuo vinavyopatikana mkoani Morogoro. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa misimu huibuka katika jamii kutokana na mabadiliko ya kihistoria ambayo hutokea kwa upande wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Anasema kuwa mabadiliko ya kisiasa huibuka na misimu mbalimbali. Mtaalamu huyu anathibitisha madai hayo kupitia mifano ifuatayo: *kutumbua majipu*, *mwendokasi* na *ukawa*. Aidha, anabainisha misimu inayopatikana katika mitandao ya kijamii kutokana na uwanja wa uchumi. Mifano ya misimu iliyoibuka katika mitandao ya kijamii kwa sababu za kiuchumi ni pamoja na: *chakachua* na *hapa kazi tu*. Malima (2018) amechunguza pia misimu iliyo katika mitandao ya kijamii akiangazia uwanja wa jamii. Kwa upande wa misimu ya kijamii, mtafiti anatoa mifano kama vile: *kutafuta kiki*, *kuperuzi*, *muziki wa kizazi kipya*, *mademu*, *dada poa*, *mrupo*, *kibendi*, *zombi*, *zege*, *kuzingua* na *kilaza*.

Licha ya suala la misimu kuangaziwa na Malima (keshatajwa) kwa kuwachunguza wanafunzi wa vyuo vikuu vya Morogoro huku akijikita katika misimu ya mtandaoni, bado inatoa nafasi ya suala hilo kuchunguzwa katika vyuo vikuu vingine kwa kujikita katika matumizi ya misimu hiyo kwenye mazingria halisi na sio mitandanoni. Aidha, kwa kuangazia suala hilo katika vyuo vikuu vilivyopo katika mikoa mingine tofauti na Morogoro itatoa picha ya jumla kuhusu matumizi ya misimu katika vyuo vikuu nchini Tanzania. Hivyo, makala hii sasa inaangazia suala hilo kwa wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilichopo Dar es Salaam, Tanzania

ambapo uchunguzi umefanywa kwa wanafunzi kwa kujikita katika matumizi yao wakiwa chuoni.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Data za makala hii imechambuliwa kwa kuongozwa na Nadharia Jumuishi ya Giles (1979). Kwa mujibu wa nadharia hii, utambulisho wa jamii au mtu ni mchakato endelevu unaohusisha vibainishi vingi. Vibainishi hivi vinadumishwa na jamiilugha. Tunapoongelea jamiilugha tunalenga mila, desturi pamoja na utamaduni. Nadharia hii inafafanua pia kuwa, jamiilugha inaundwa na watu wanaojitambua kuwa wanatokana na jamiilugha moja iliyo tofauti na jamiilugha nyingine. Aidha, jamiilugha kwa mujibu wa nadharia hii ni msingi mkubwa wa maana halisi ya utambulisho na ni msingi mkuu wa nadharia hii kwa ujumla. Zipo maana halisi mbili za utambulisho, ya kwanza ni jamiilugha husika kuweza kujitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine kimila, kidesturi, kiutamaduni pamoja na kiimani. Msingi huu wa utambulisho ni msingi unaoiwezesha jamiilugha kudumisha mila, desturi, utamaduni pamoja na imani yao. Pili, ni wanajamiilugha husika kuthamini vibainishi vya msingi vinavyowatofautisha na wanajamiilugha wengine pamoja na kuithamini lugha yao.

### 2.1 Jinsi Nadharia Ilivyoongoza Utafiti wa Makala Hii

Nadharia Jumuishi ya Giles (1979) imekuwa muafaka katika utafiti wa makala hii kutokana na misingi yake mikuu. Msingi wa kwanza unaeleza kuwa, utambulisho wa jamii au mtu ni mchakato endelevu unaohusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamiilugha husika. Jamiilugha inayoongelewa katika nadharia hii inahusisha mila, desturi na utamaduni. Msingi wa pili unafafanua kuwa, jamiilugha inaundwa na watu wanaojitambua wenyewe kuwa wanatokana na jamiilugha moja iliyo tofauti na jamiilugha nyingine. Misingi hii imetuongoza kutambua kuwa jamiilugha ya wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambapo jamii hiyo hudumisha mila, desturi, utamaduni pamoja na imani zao katika mawasiliano yao ya kila siku. Vilevile, jamii hiyo hutambua kuwa jamii yao ni tofauti na jamiilugha nyingine kimila, kidesturi, kiutamaduni pamoja na kiimani kutokana na lugha wanayoitumia. Aidha, imetusaidia kutambua kuwa wanajamiilugha hawa huthamini vibainishi vya msingi vinavyowatofautisha na wanajamiilugha wengine pamoja na kuithamini lugha yao.

## 3.0 Methodolojia

Data ya makala hii imechanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli au maelezo. Mkabala wa kitaamuli au maelezo hujihusisha zaidi na maelezo katika utafiti hususani katika uchambuzi wa data (Walliman, 2008). Mkabala wa kitaamuli umetumika kwa msingi kuwa yametumika maelezo na ufafanuzi katika ubainishaji wa misimu mbalimbali itumiwayo na wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Kwa upande wa eneo la mada ya utafiti, mtafiti ameteua nyanja tatu tu, uwanja wa taaluma, uchumi pamoja na jamii. Sababu ya kuteua nyanja hizi ni kwamba si rahisi kutafiti maeneo yote inamotumika misimu kutokana na sababu ya ufinyu wa muda na bajeti iliyopangwa na mtafiti wa makala hii. Ili kulishughulikia eneo hili kwa kina, mtafiti hakujihusisha na maeneo mengine kama vile sanaa, soka, siasa na mitandao ya kijamii. Halikadhalika, sampuli ya makala hii ilijumuisha watoa taarifa (ambao ni wanafunzi) 20 walioteuliwa na mtafiti kwa minajili ya kutimiza malengo ya kiutafiti.

Miongoni mwa watoa taarifa hawa 20, wa kike walikuwa 10 na wa kiume walikuwa 10. Mtafiti ameteua vijana kwa kuwa ni rika linaloonekana kupenda kutumia misimu zaidi kuliko rika lingine katika mawasiliano kwenye jamii. Ili kupata sampuli hii, mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Kupitia mbinu hii, sampuli huchaguliwa kwa uhuru wa mtafiti ili kupata data inayosaidia kujibu maswali ya utafiti. Aidha, kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliteua watoa taarifa, nyaraka mbalimbali kama vile, vitabu, tasinifu, maandiko tofautitofauti pamoja na majarida kama vyanzo vikuu vya data ya makala hii. Aidha, kupitia mbinu hii mtafiti alipata sampuli ya wanachuo waliompatia taarifa zilizohusiana na misimu ya kitaaluma, kiuchumi na kijamii inayoshughulikiwa katika makala hii.

Mtafiti amekusanya data ya makala hii kwa kutumia hojaji pamoja na usaili. Hojaji ilihusisha orodha ya maswali na maelekezo yaliyoandaliwa na mtafiti ili yaweze kujibiwa na watoa taarifa kwa lengo la kukusanya data ya utafiti. Mbinu ya hojaji iliteuliwa katika makala hii kwani mbinu hii humpa mtoa

taarifa uhuru wa kutoa majibu bila woga. Pia, hojaji huweka ulinganifu wa majibu yanayotolewa na watoa taarifa wote. Wanachuo 20 walijaza hojaji ambapo mtafiti alihitaji orodha ya misimu mbalimbali wanayoitumia chuoni kwao. Halikadhalika, mtafiti ametumia usaili kama mbinu ya kupata data ya makala hii. Mbinu ya usaili imewafaa watoa taarifa kwani ni ya muda mfupi na haimlazimu mtoa taarifa kutumia muda mrefu kwa ajili ya kusoma na kuandika.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya makala yanaonesha kuwa ipo misimu kadhaa inayotumiwa na watoa taarifa. Nyanja zinazoshughulikiwa katika kipengele hiki ni nyanja za taaluma, uchumi pamoja na jamii. Data kutoka katika mbinu zote za ukusanyaji zimechujwa na kuwasilishwa pamoja kama zinavyoonekana katika jedwali la 1-3.

### 4.1 Misimu Inayohusiana na Taaluma

Data ya makala hii iliyokusanywa kwa mbinu ya hojaji na usaili, inaonesha kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu mbalimbali inayohusiana na taaluma. Taaluma ni ujuzi wa fani fulani ambao hupatikana kutokana na mafunzo maalumu ya elimu. Massamba (2016) anafasili dhana ya taaluma kama tawi la maarifa ambalo hushughulikia ujuzi au elimu fulani maalumu. Watoa taarifa wa makala hii hutumia misimu inayohusiana na uwanja wa taaluma pale wanapowasiliana katika maisha yao ya kila siku. Kwa ujumla uwanja huu una misimu mingi kwani ndiyo muhimili mkuu na ndilo lengo lao kubwa la kuwa chuoni hapo. Mifano ifuatayo inathibitisha zaidi:

**Jedwali Na. 1: Misimu Inayohusiana na Taaluma**

| Misimu ya Masomo | Maana ya Misimu |
|---|---|
| *Bundi/kubundi* | Jina analopewa mwanachuo anayetumia muda mwingi kujisomea. Kubundi ni tendo la baadhi ya wanachuo kujishughulisha na masuala ya kujisomea ambapo hutumia muda mwingi katika jambo hilo kuliko muda unaotumika katika shughuli nyinginezo. |
| *Chabo* | Hali ya kuibia majibu kwenye mtihani kwa kuangalizia majibu ya wanachuo au wanafunzi wengine. Wizi huu unaweza kufanyika pia kutoka chanzo kingine kisichoruhusiwa katika chumba cha mtihani. Kwa mfano, kujiandika mwilini, kuacha maandishi vyooni, kuingia na daftari au kitu chochote chenye maandishi yanayohusiana na somo linalofanyiwa mtihani. |
| *Desa* | Nyaraka za kusoma kama vile daftari, vitini nakadhalika. |
| *Ibia* | Wizi wa majibu ya mitihani. Mwanachuo anaweza kuiba kutoka kwa mwanachuo aliyekaa jirani yake au kutoka kwenye simu, daftari, karatasi, 'smart watch' nakadhalika, wakati wa kufanya mtihani. Msimu huu ni sawa na msimu chabo. |
| *Jembe* | Mwanachuo anayejitahidi katika masomo, ujengaji wa hoja na huwa na wastani wa juu katika matokeo ya mitihani. Pia anaweza kuwa kinara katika kuchapa kazi, kupanga mipango ya kimaisha na kuitekeleza vema nakadhalika. |
| *Kilaza* | Mwanachuo asiyekuwa na juhudi katika masomo, ujengaji wa hoja na mara nyingi hupata alama za chini katika masomo. Kwa ujumla ni mwenye kiwango cha chini katika kufikiri, kuchapa kazi, kupanga mipango ya kimaisha na kuitekeleza. |
| *Kipanga* | Mwanachuo mwenye juhudi katika masomo, hujenga hoja zenye mashiko na alama zake za mitihani ni za juu tofauti na kilaza. Pia msimu huu hutumiwa na wanachuo kuwaita wahadhiri wanaojiamini katika suala zima la ufundishaji na wanaoyamudu vema masomo au kozi wanazofundisha. |

| Misimu ya Masomo | Maana ya Misimu |
|---|---|
| *Kitini* | Kijitabu chenye kurasa chache chenye kuelekeza juu ya somo au kozi fulani. (*Handout/pamphlet*) |
| *Tango pori* | Ufafanuzi usio sahihi wa kile kinachofafanuliwa. Au fasili isiyo sahihi kwa kile kinachofasiliwa. |
| *Zima moto* | Tendo la wanachuo kusoma mambo mengi kwa muda mfupi kipindi cha mitihani. Hii ni kutokana na kutojiandaa vyema kabla ya kipindi cha kufanya mitihani husika. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani (2022)

Mifano iliyotolewa katika Jedwali Na. 1 inathibitisha kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu inayohusiana na uwanja wa taaluma. Miongoni mwa misimu inayotumiwa ni pamoja na neno *bundi*. Hili ni jina wanalopewa wanachuo wanaozingatia vema muda wao katika suala zima la kusoma. Wanachuo hawa hutumia muda mrefu mathalani hujisomea katika maktaba, hosteli, darasani, katika mazingira ya chuo na hata katika nyumba zao wanakoishi. Aidha, msimu *kubundi* ni tendo la wanachuo kutumia muda mrefu kujisomea. Data ya makala hii inathibitisha pia kuwa msimu *chabo* hutumiwa na watoa taarifa wa makala hii. Msimu huu hurejelea hali ya kuiba majibu kwenye mtihani kwa kuangalizia majibu ya mwanachuo au wanachuo wengine. Yaweza kuwa makubaliano ya anayeiba na anayeibiwa au bila makubaliano, yaani anayeiba hufanya hivyo bila ridhaa ya mhusika hasa mhusika asipokuwa makini na karatasi au kijitabu chake cha kujibia. Msimu mwingine uliyotokana na data ya makala hii ni *desa*. Kama ilivyofasiliwa hapo juu, *desa* hurejelea nyaraka mbalimbali zinazotumiwa na wanachuo katika somo au kozi husika. Nyaraka hizo ni pamoja na: daftari, vitini na kadhalika. Kwa hiyo, wanachuo hutumia msimu *desa* kama mbadala wa daftari, kitini na kadhalika.

Aidha, wanachuo hutumia msimu *ibia* kwa kuficha ukali wa neno kuiba. Hali hii hujitokeza kwa wanachuo wanaoingia katika vyumba vya mitihani pasipokuwa na maandalizi ya kutosha. Hii huwapelekea kuiba majibu kwa wenzao, kuingia na maandishi yanayohusiana na somo linalofanyiwa mtihani au kuficha maandishi hayo vyooni. Wanafunzi walioficha maandishi hayo vyooni, hujifanya wanaomba ruhusa ya kwenda haja ilhali wanaenda kuiba

majibu. Kama haitoshi, wengine huandika majibu ya somo husika mapajani, kwenye viganja na sehemu nyingine za miili yao. *Jembe* pia ni mojawapo ya msimu unaotumiwa na watoa taarifa wa makala hii. Kama ilivyodadavuliwa hapo juu, pale wanachuo wanapotumia msimu huu katika muktadha wa chuoni humaanisha mwanachuo mwenye juhudi katika masomo, mwenye uwezo wa kufikiri na kujenga hoja na huwa na ufaulu wa juu katika matokeo ya mitihani. *Kilaza* ni msimu ulioonekana kushika kasi miongoni mwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Wanachuo wanaposema fulani ni *kilaza* maana yake tabia zake ni kinyume na *jembe*. Yaani, ni mwanachuo asiye na juhudi katika masomo, ana uwezo mdogo wa kufikiri, au ana uwezo mdogo kimasomo na katika kujenga hoja na huwa na ufaulu wa chini katika matokeo ya mitihani.

Kupitia mbinu ya usaili ya utafiti wa makala hii, imethibitika kuwa watoa taarifa wa makala hii huwasiliana kwa kutumia msimu *kipanga* katika uwanja wa taaluma. Kama ilivyoelezwa katika Jedwali Na. 1 kuwa *kipanga* ni mwanachuo mwenye juhudi katika masomo; hujenga hoja zenye mashiko na alama zake za mitihani ni za juu tofauti na *kilaza*. Aidha, kwa upande wa wahadhiri, *kipanga* ni mhadhiri anayejiamini, anayefundisha vizuri, anayetoa hoja madhubuti na ni yule anayelimudu somo au kozi yake vilivyo. Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia msimu *kitini*. Msimu huu hurejelea kijitabu chenye kurasa chache na ni mhutasari wa somo au kozi fulani. Wakati mwingine wanachuo hukiita *kitini* majina ya Kiingereza kama: *handout* au *pamphlet*. Pamoja na misimu hii, ipo mingine kama vile, *tango pori*. *Tango pori* ni hali ya kufafanua jambo tofauti na jinsi lilivyo au fasili tofauti na dhana husika. Mwanachuo au mtu yeyote akifafanua dhana fulani au jambo tofauti na inavyotarajiwa au tofauti na maana yake halisi, wanachuo hao husema kuwa ametulisha *tango pori*. Halikadhalika, kupitia mbinu ya hojaji, watoa taarifa wa makala hii wameeleza kuwa hutumia msimu *zima moto* katika suala zima la kupata elimu wakiwa chuoni. Hili ni tendo la wanachuo kusoma mambo mengi kwa muda mfupi kipindi cha mitihani. Hii ni kutokana

na kutojiandaa vyema na mitihani hiyo kabla ya siku za kufanya mitihani pindi wawapo chuoni.

### 4.2 Misimu Inayohusiana na Uchumi

Kupitia mbinu ya usaili na hojaji, imethibitika wazi kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu inayohusiana na uwanja wa uchumi. Tunapozungumzia uchumi, tunarejelea jumla ya shughuli zinazofanywa na mtu binafsi au kundi la watu ili kukidhi mahitaji yao. Misimu ya kiuchumi itumiwayo na watoa taarifa imeoneshwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Misimu Inayohusiana na Uchumi**

| Misimu ya Uchumi | Maana ya Misimu |
|---|---|
| *Boom* | Kiuhalisia hiki ni kipindi ambacho wanufaika wa mkopo (wanachuo) hupokea au hupata fedha ya kujikimu kutoka bodi ya mikopo. Isipokuwa wanachuo hutumia msimu huu kurejelea hela wanayokopeshwa kutoka Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kujikimu. |
| *Buku* | Fedha yenye thamani ya shilingi elfu moja. |
| *Jero* | Fedha yenye thamani ya shilingi mia tano. |
| *Limetema* | Tendo la bodi ya mikopo kuwawekea fedha wanachuo kwenye akaunti zao. |
| *Mawe, mpunga au mshiko* | Vyombo vya kubadilishana bidhaa vyenye thamani kubwa mathalani fedha, hela au pesa. |
| *Pambana na hali yako* | Msimu utumikao kumtaka mtu akabiliane na changamoto anazokumbana nazo hasahasa kutokana na hali ngumu ya kiuchumi. |
| *Pasi ndefu* | Tendo la wanachuo ama kulala njaa, kushinda njaa au kutokupata kifungua kinywa (kukosa kimojawapo kati ya hivyo). Hali hii yaweza kujitokeza kwa sababu ya kukosa fedha au kukosa muda wa kula kutokana na kubanwa na ratiba ya masomo. Lakini mara nyingi ni ukosefu wa fedha ya kuweza kununulia chakula cha milo yote mitatu kwa siku. |
| *Sponsa* | Mtu anayegharamikia mahitaji ya mtu mwingine, kumfadhili mpenzi wake katika mahitaji yake ya kila siku mathalani, kumlipia ada, kumpangishia nyumba na kadhalika. |
| *Vyuma vimekaza* | Hali ngumu ya kiuchumi au kuadimika kwa fedha. |
| *Zero zero one (001)* | Tendo la wanachuo kutokupata kifungua kinywa na chakula cha mchana. Yaani hula mlo mmoja tu kwa siku kwa sababu ya kukosa fedha ya kutosha kwa ajili ya manunuzi ya chakula cha |

| Misimu ya Uchumi | Maana ya Misimu |
|---|---|
| | milo yote mitatu kwa siku. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani (2022)

Kutokana na data iliyo katika Jedwali Na. 2, ni dhahiri kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu mbalimbali inayohusiana na uchumi pindi wawapo chuoni hapo. Tunaona kuwa uwanja wa uchumi ni mojawapo ya nyanja kadhaa zilizosheheni misimu katika chuo kilichomakinikiwa. Mathalani, msimu *boom* umeshika kasi miongoni mwa watoa taarifa. Msimu huu unatumika mara nyingi kwani ndiyo mhimili mkuu wa kiuchumi unaowasaidia kuendesha maisha yao pindi wawapo chuoni kimasomo. Kwa mujibu wa watoa taarifa wa makala hii, msimu *boom* ni hela wanayokopeshwa na bodi ya mikopo kwa ajili ya kujikimu. Isipokuwa wamefafanua kuwa, kiuhalisia *boom* ni kile kipindi ambacho wanufaika wa mkopo ambao ni wanachuo hupokea au hupata fedha ya kujikimu kutoka bodi ya mikopo. Kwa hiyo, badala ya kukipa kipindi hicho jina la *boom* wametoa jina hilo kwa fedha wanayopewa na bodi ya mikopo kwa ajili ya kujikimu. Aidha, msimu *buku* hutumiwa sana na wanachuo wakiwa chuoni hapo ambapo kwa kusema hivyo humaanisha kiasi cha fedha ambacho thamani yake ni hela ya Kitanzania shilingi elfu moja. Kutokana na maelezo waliyotoa ni kwamba, wao hupendelea kutumia msimu wa *buku* kuliko msamiati ‘elfu moja’. Pamoja na msimu huo, mwingine unaohusiana na fedha ni msimu *jero*. *Jero* kama ilivyofafanuliwa hapo juu hurejelea kiasi cha shilingi mia tano, hela ya Kitanzania. Data ya makala hii inathibitisha kuwa msimu huu hutumiwa zaidi tofauti na jinsi ambavyo kisawe chake hutumika. Kisawe cha msimu huu ni shilingi mia tano. Aidha, katika uwanja huu wa uchumi, wanachuo hutumia msimu, *limetema*. Hutumia msimu huu wakirejelea tendo la kuingiziwa fedha kwenye akaunti zao kutoka bodi ya mikopo. Hii huwa ni hali ya neema kwao na ndiyo maana ikawafanya kuzua msimu huo. Vilivile, msimu *mawe* unatumiwa na watoa taarifa wa makala hii ukirejelea fedha. Mara chache watoa taarifa hutumia msamiati fedha, hela au pesa ikilinganishwa na msimu *mawe* ambao hutumiwa mara nyingi.

Aidha, matokeo ya makala hii yamebainisha kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia msimu *mpunga* katika mawasiliano yao ya kila siku. Wanachuo hawa wakisema fulani hana *mpunga* wa kutosha humaanisha kuwa mtu huyo hana fedha ya kutosha. Katika uwanja huu wa uchumi, pia msimu *mshiko* umeonekana kutumika kwa kiwango kikubwa chuoni hapo. Msimu huu hauna tofauti na *mpunga* na *mawe*. Yote herejelea fedha au kitu chenye thamani kubwa cha kubadilishana na bidhaa katika jamii. Hivyo, mwanachuo akisema; 'kwa hivi sasa sina *mshiko'*, maana yake hana fedha. Kupitia mbinu ya hojaji ya ukusanyaji data ya makala hii, watoa taarifa wameeleza kuwa hali ngumu ya kiuchumi imesababisha kuzuka kwa msimu *pambana na hali yako.* Kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali Na. 2, msimu huu hutumika miongoni mwa watoa taarifa wa makala hii. Wamefafanua kuwa msimu *pambana na hali yako* humaanisha ya kwamba ni muhimu mtu kuwa na stamina ya kukabiliana na hali ngumu ya maisha na kutafuta namna ya kuondokana nayo hasa pale anapokumbana na ugumu wa kiuchumi.

Halikadhalika, msimu *pasi ndefu* umeonekana kutumika mara nyingi chuoni hapo. Hali hii hujitokeza kwa sababu ya ukosefu wa pesa au hata kukosa muda wa kula kutokana na kubanwa na ratiba ya masomo. Kwa mujibu wa maelezo ya watoa taarifa wa makala hii ni kwamba msimu huu hutumika sanasana kutokana na hali ya kukosa fedha ya kununulia chakula cha kutosha kwa milo yote mitatu kwa siku. Msimu *pasi ndefu* ni tendo la mwanachuo kukosa mlo mmojawapo kati ya milo mitatu ya siku. Yaani, kukosa kimojawapo kati ya: kifungua kinywa, mlo wa mchana au wa usiku. Hali hii hujitokeza pale wanachuo wanapokuwa katika kipindi cha ukata, yaani hawana fedha ya kujikimu. Hivyo, huwasababishia kutokula baadhi ya milo inayotakiwa kuliwa kwa siku. Halikadhalika, s*ponsa* ni msimu utumiwao na wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wakirejelea mtu kumfadhili mpenzi wake au kumgharimikia katika mahitaji mbalimbali kama vile: kumpangishia nyumba, kumlipia ada, kumnunulia mavazi, chakula, kumpatia pesa za kujikimu, na kadhalika.

Msimu mwingine ulioonekana kutumika katika uwanja wa uchumi chuoni hapo ni *vyuma kukaza*. Kwa mujibu wa mbinu ya usaili, watoa taarifa wa makala hii wameeleza kuwa msimu huu umeshika kasi chuoni hapo. Wanasema kuwa msimu huu humaanisha hali ngumu ya maisha na hasa kifedha. Kwa mujibu wa data ya makala hii, msimu huu umetokana na ugumu wa maisha uliozuka katika kipindi cha uongozi wa awamu ya tano hapa nchini Tanzania. Katika kipindi hiki cha uongozi hela ilipatikana kwa tabu sana na kusababisha hali ya maisha kuwa ngumu. Kutokana na kuadimika kwa fedha, biashara zilidorora; hoteli, maduka, migahawa mikubwa, na kadhalika vilifungwa kutokana na kodi kupanda na hivyo wafanyabiashara kushindwa kuendesha biashara mbalimbali. Aidha, data ya makala hii inadhihirisha kuwa, msimu *vyuma vimekaza* ulitokana pia na watumishi hewa kufukuzwa kazi, posho za vikao kupunguzwa na kadhalika. Hivyo, wanachuo hutumia msimu huu wakimaanisha hali ngumu ya maisha wanayokumbana nayo hususan hali ngumu ya kiuchumi. Uwanja huu pia umeonekana kuwa na msimu *zero zero one* (*001*). Tofauti na msimu *pasi ndefu* ambapo wanachuo hukosa mlo mmoja, kwa mfano, kupata kifungua kinywa na kutokula chakula cha mchana, au kula chakula cha mchana na kulala njaa au kula usiku na kutokupata kifungua kinywa na kupata mlo wa mchana tu, msimu *zero zero one* ni tofauti. Msimu *zero zero one* (*001*) ni tendo la baadhi ya mwanachuo kukosa milo miwili na kupata mlo mmoja tu kwa siku. Hapa hapati kifungua kinywa na chakula cha mchana; hivyo, anakula mlo mmoja tu wa usiku. Mbali na wanachuo kutumia misimu ya nyanja za taaluma na uchumi, pia hutumia misimu katika uwanja wa kijamii. Tuone ni kwa namna gani misimu hiyo hutumiwa na wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere:

### 4.3 Misimu ya Kijamii

Mbinu ya hojaji na usaili zilizotumika kukusanyia data ya makala hii zinathibitisha kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu ya kijamii katika mawasiliano yao ya kila siku. Hii ni kutokana na wanachuo hawa kutangamana na wanajamii mbalimbali. Jamii hurejelea mkusanyiko wa watu waishio pamoja. Watu hawa huwa katika eneo

moja la kijiografia na huwa na historia, utamaduni, shughuli za kiuchumi pamoja na mila na desturi zinazoendana. Mifano iliyotolewa katika Jedwali Na. 3 inadhihirisha kuwapo kwa misimu ya kijamii.

**Jedwali Na. 3: Misimu ya Kijamii**

| Misimu ya Kijamii | Maana ya Misimu |
|---|---|
| *Damshi* | Kuwa na mwonekano wa kupendeza, mathalani kimavazi na mapambo mengine ya kumfanya mtu apendeze. |
| *Hatupoi* | Kauli inayoonesha utayari wa watu katika kufanya jambo fulani au kuendelea kutimiza wajibu unaowakabili kwa ufanisi wa hali ya juu. |
| *Kausha* | Tendo la kumnyamazisha mtu au kumzuia kutenda tendo fulani. |
| *Kibenteni* | Mtoto wa kiume anayependa wanawake waliomzidi umri. Lengo na nia ya kufanya hivyo ni kutaka kutimiziwa mahitaji yake yote na mwanamke huyo. |
| *Kula tano* | Hali ya kuonesha kukubaliana na mawazo au kuunga mkono mawazo ya mtu fulani. |
| *Kupigwa na kitu kizito* | Kupata pigo fulani la kuhuzunisha. |
| *Mcharu au mcharuko* | Mtu ambaye hajatulia na ambaye tabia zake ni za hovyohovyo. Pia, tabia za mtu huyu ni za utundu usiyo na faida. Aidha, hujulikana kama kicheche. |
| *Mchepuko/michepuko* | Hawara au watu wenye mahusiano ya kimapenzi pasipo kufunga ndoa au pasipo kuishi pamoja kama mume na mke halali. |
| *Mtoto mayai au mtoto wa mama* | Watu wasiotaka kujishughulisha katika maisha. Hupenda kufanyiwa kila kitu mathalani, kupikiwa, kufuliwa nguo, kufanyiwa kazi za darasani, na kadhalika. Watu wa namna hii huwa na deko lililopitiliza kwani hawapendi kujishughulisha na shughuli yoyote ile isipokuwa kwa kulazimishwa. |
| *Pisi kali* | Msichana mzuri sana au mrembo. |
| *Povu* | Maneno yanayomtoka mtu baada ya kukasirika. |
| *Tuliza mshono* | Tulia, acha makeke. |
| *Tuna jambo letu* | Msimu utumikao kwa watu wanaokuwa na shughuli maalumu. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani (2022)

Mbinu ya hojaji na usaili katika makala hii zinabainisha kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wanatumia misimu mingi inayotokana na jamii. Iliyotolewa katika Jedwali Na. 3 ni baadhi tu ya misimu

hiyo. Misimu hii hubeba maana kadhaa katika mawasiliano yao ya kila siku. Kwa mfano, msimu *damshi* humhusu mtu aliyependeza kimwonekano kuanzia mwili hadi mavazi yake. Aidha, msimu *hatupoi* hutumika miongoni mwa watoa taarifa wa makala hii. Kwa kutumia msimu huu vijana huonesha hali ya kuchapa kazi kama mchwa. Pia, msimu huu hufanana na msimu usemao *kazi iendelee, hakuna kulala, kazikazi* na kadhalika ambayo humaanisha watu kuwa na raghba ya kuendelea kufanya kazi au kutimiza majukumu yanayowakabili.

Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa msimu *kausha* hutumika miongoni mwa watoa taarifa wa makala hii. Msimu huu hurejelea tendo la kumkataza mtu asifanye tendo fulani au kuongelea suala fulani. Msimu mwingine wa kijamii ulioonekana kutumika miongoni mwa watoa taarifa wa makala yetu kutokana na data iliyokusanywa ni ule ujulikanao kama *kibenteni*. Mtu akiitwa kwa jina hili maana yake ni kwamba anaishi kwa kutegemea kutunzwa au kutimiziwa mahitaji yake ya kimaisha na mtu ambaye wako katika mahusiano ya kimapenzi. *Vibenteni* hupenda kutunzwa kwa kila kitu maishani mwao, mathalani walishwe, wavalishwe, wapewe hela ya matumizi, watibiwe na mambo mengine kama hayo. Na hawa ni watoto wa kiume wanaowapenda akina mama au wanawake waliowazidi umri. Msimu mwingine ni *kula tano*. Msimu huu humaanisha kuungwa mkono kwa kile kilichosemwa au kutendwa. Pamoja na misimu hiyo, upo pia ule usemao: *tumepigwa na kitu kizito*. Kupitia mbinu ya usaili iliyotumiwa na mtafiti wa makala hii, watoa taarifa wameeleza kuwa huu ni msimu unaotumiwa chuoni hapo mara nyingi. Sababu za kutumika mara nyingi kwa msimu huu ni kutokana na hali ngumu wanayopitia wanachuo hao wakiwa katika harakati za kusaka elimu. Hivyo, pale wanapokumbana na changamoto mbalimbali husema *tumepigwa na kitu kizito*. Kwa mfano, kupata alama ndogo za tamrini, kufanyishwa mtihani wa kushtukizwa, ratiba ya mtihani kubananishwa, kurudia masomo baada ya kushindwa kufikisha alama zinazotakiwa na mambo mengine kama hayo.

Pamoja na misimu hiyo ya kijamii pia kuna msimu kama vile *mcharuko* au *mcharu*. Huu ni msimu unaotumika kwa watu wenye tabia ya utundu. Utundu

huu siyo ule wenye faida na wala hauna tija katika jamii isipokuwa ni wa hovyo tu ambapo huishia kuwaletea sifa mbaya wahusika na hauwanufaishi. Watu wa namna hii pia huitwa 'mapepe' au 'vicheche'. Katika uwanja huu pia tumepata msimu: *mchepuko*. Mchepuko ni jina wanalopewa watu wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi yasiyo rasmi yaani kuishi kama mke na mume isivyo halali. *Mtoto mayai* au *mtoto wa mama* pia ni mojawapo ya misimu iliyopatikana kutoka kwa watoa taarifa wa makala hii. Haya ni majina wanayopewa watu wasiotaka kujishughulisha. Watu wa namna hii hupenda kufanyiwa kila kitu, mathalani kufuliwa, kupikiwa, kufanyiwa kazi za darasani na kadhalika. Kwa ujumla hawataki shida. Pia, data ya makala hii inaonesha kuwa *pisi kali* ni miongoni mwa misimu iliyoshika kasi katika nyakati hizi za miaka ya 2021 na 2022. Hili ni jina wanalopewa wasichana warembo, yaani wenye mwonekano mzuri wa kuanzia sura na umbo la mwili kwa ujumla.

Halikadhalika, katika jamii kuna mambo mengi, mojawapo ikiwa ni utani, pongezi, kusifiana, kejeli, matusi, dharau na mambo mengine ya mlengo huo. Hii ni kutokana na jamii kuwa na mkusanyiko wa watu wenye tabia, malezi, makuzi na hadhi tofauti. Kutokana na hayo, ni dhahiri kuwa wapo watu wenye tabia ya kusifia, kutia moyo, kusaidia na kuwavusha wanajamii kimaendeleo. Lakini pia wapo ambao kawaida yao ni kuwaudhi wenzao, kuwadharau, kuwatukana, kuwakejeli na kuwachokoza hali inayowapelekea wenzao kukasirika na kutoa maneno machafu au matusi. Hali ya mtu kutokwa na maneno machafu na matusi mara afanyiwapo maudhi yaliyoorodheshwa hapo juu, huambiwa kuwa *anatoa povu*. Kwa hiyo, tendo la mtu kukemea au kujitetea pengine kwa kutumia lugha kali pale anapoudhiwa, kuchokozwa au kufanyiwa jambo lisilompendeza, hujulikana kama *kutokwa na povu*. Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa wanachuo hutumia msimu *tuliza mshono* ambao wameupata kutoka katika jamii wanamoishi. Huu ni msimu usiopendeza kwa mhusika kwani ni namna ya kumzuia kufanya jambo fulani; hasahasa hutumika kumnyamazisha mtu. Msimu *tuliza mshono* umekaakaa kimatusi tofauti na msimu *kausha*. Msamiati mzuri unaoweza kutumika badala ya msimu *tuliza mshono* ni acha, nyamaza tu, tulia na kadhalika.

Msimu *tuna jambo letu* unatumiwa na watu wengi katika jamii, jambo ambalo limewafanya wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuutumia kwa wingi. Huu ni msimu unaotumiwa na wanachuo pale ambapo hupaswa kutimiza wajibu fulani na hata mambo yao wanayohitaji kuyajadili au pale wanapokuwa na tafrija fulani. Basi msimu huu hutumika katika mazingira kama hayo.

## 5.0 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya data ya makala hii, ni dhahiri kuwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hutumia misimu ya nyanja mbalimbali. Miongoni mwa nyanja zilizoshughulikiwa katika makala hii ni uwanja wa taaluma, uchumi pamoja na jamii. Katika uwanja wa taaluma tumeona misimu kama: *bundi*, *chabo*, *desa*, *ibia*, *jembe*, *kilaza*, *kipanga*, *kitini*, *tango pori* pamoja na *zima moto.* Uwanja wa uchumi umebainika kuwa na misimu kadha wa kadha. Tuone baadhi ya misimu tuliyoijadili: *boom*, *buku*, *jero*, *limetema*, *mawe*, *mpunga*, *mshiko, pambana na hali yako*, *pasi ndefu*, *sponsa*, *vyuma kukaza* na *zero zero one (001)*. Aidha, imebainika kuwa uwanja wa jamii umesheheni misimu inayotumiwa na wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Misimu iliyotokana na uwanja huu ni pamoja na *damshi*, *hatupoi*, *kausha*, *kibenteni*, *kula tano*, *kupigwa na kitu kizito kichwani*, *mcharuko* au *mcharu*, *mchepuko*, *mtoto mayai* au *mtoto wa mama*, *pisi kali*, *povu*, *tuliza mchono* pamoja na *tuna jambo letu*. Kwa ujumla, nyanja za taaluma, uchumi na jamii zimechangia kwa kiasi kikubwa kwa watoa taarifa wa makala hii ambao ni wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kupata misimu mbalimbali kama ilivyobainishwa katika makala hii. Kutokana na mifano iliyobainishwa kutoka katika nyanja hizo ni uthibitisho tosha kuwa watoa taarifa hao hutumia misimu katika mawasiliano yao ya kila siku. Kutokana na kubainika kwa matumizi ya misimu hiyo lukuki, ni dhahiri kwamba watoa taarifa hawa wana mchango mkubwa katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili kwa kukiongezea msamiati. Aidha, kwa kuwa wanachuo ni sehemu ya jamii bila shaka jamii imechangia kwa kiasi kikubwa kwa wanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuwa na misimu mbalimbali kama ilivyodadavuliwa katika makala hii.

Hii ni kutokana na sababu kuwa baadhi ya misimu iliyoshughulikiwa na mtafiti wa makala hii itashika mizizi na kusanifishwa jambo litakaloiongezea msamiati lugha ya Kiswahili. Makala hii imesaidia kubainisha misimu kadhaa kutoka katika nyanja za taaluma, uchumi pamoja na jamii.

## 6.0 Mapendekezo

Kwa kuwa misimu ni moja ya vyanzo vya ukuzaji wa msamiati, makala hii inapendekeza kwamba vyombo vinavyohusika na uratibu wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali kama vile BAKITA, BAKIZA na TATAKI vichukue misimu hii na kuitathmini kisha kubaini ile inayoweza kusanifishwa. Aidha, kwa kuwa makala hii imechunguza misimu inayohusiana na taaluma, uchumi na jamii tu inapendekezwa kwamba tafiti zijazo zichunguze misimu ya nyanja nyingine kama vile sanaa, soka, siasa, dini, na kadhalika. Vilevile, mtafiti wa makala hii anapendekeza maeneo mengine tofauti na eneo la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere yafanyiwe utafiti kuhusiana na suala zima la misimu. Maeneo hayo yanaweza kuwa vituo vya mabasi, vijiwe vya kuuzia nguo, vijiwe vya wapiga debe wa magari, sokoni, migodini na maeneo mbalimbali ili kubaini ni misimu gani inatumika katika maeneo hayo.. Mtafiti anapendekeza pia kuwa wanachuo waache tabia ya kutumia misimu ya matusi, kejeli, dharau na kubeza kwani jambo hili halipendezi miongoni mwa wasomi na jamii kwa ujumla. Aidha, misimu ya namna hii huwavunja moyo wanajamii na kuwafanya baadhi yao wajisikie vibaya kwa kuona kuwa wanadharauliwa, kubezwa na kutukanwa. Pia, misimu ya namna hiyo huweza huzua ugomvi na mitafaruku miongoni mwa wanajamii. Halikadhalika, imethibitika pasi na shaka kwamba misimu ya namna hii haina manufaa katika jamii; kwa mfano, Mhe. Rais wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan aliwahi kukemea msimu *kwio*. Kwa hakika msimu huu hauna maana yoyote wala faida katika jamii. Kwa hiyo, si kila msimu unaozuka katika jamii utumike; ile yenye kuondoa amani ipuuzwe ili kudumisha amani na upendo katika jamii.

## Marejeleo

Almasi, A. (2011). "Mchango wa Muziki wa Hip Hop Katika Kukuza Kiswahili", Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Dalzell, T. (2006). *Power of Slang*. London: Oxford University Press.

Giles, H. (1979). *Ethinicity Markers in Speech* katika K.R Scheres and H.Giles (eds), Social Maker in Speech. London: Cambridge University Press.

Ibrahim, A. (2012). "Matumizi ya Misimu ya vijiweni Katika lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Jiji la Dar es Salaam". Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii*. Dar -es- Salaam: TUKI.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Open University Tanzania.

Kiunga, M. T. (2016). "Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii Hususani *Facebook* na *Twitter*", Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Malima, C. (2018). "Kuchunguza Matumizi ya Misimu ya Wanavyuo Inavyotumika katika Mitandao ya Kijamii Mjini Morogoro". Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam. TUKI.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.

Njoka, A. M. (2004). *Historia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (1973). *Misemo ya Mitaani*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shayo, I. (2015). Semi Zilizoandikwa katika Maeneo ya Biashara; Uchunguzi Kuhusu Asili, Muundo, Miktadha, na Utokeaji wa

Dhima zake, Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Spears, R. A. (1991). *Slang and Euphemism*, New York: Penguin Publishers.

Thorne, M. (2015). *African American Slang*: *A Linguistic Description*. University of Cambridge. Cambridge University Press.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Presss.

Walliman, N. (2008). 'The Essential Guide for Succes'. Milton Park: Rout.